

Ahadi kumi na mbili za Moyo Mtakatfu wa Yesu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · August 3, 2020

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Huruma ya Mungu · #Katoliki: Moyo Mtakatifu wa Yesu · #Katoliki: Mungu · #Katoliki: Mwili na Damu ya Yesu · #Katoliki: Yesu Kristu

Bwana Yesu mwenyewe kwa kutumia kinywa cha Mtakatifu Margareta Maria Alakoki aliahidi Baraka na neema zifuatazo kwa wale wote watakaouheshimu Moyo wake Mtakatifu.

Na kwa maneno yake mwenyewe, Bwana Yesu aliahidi:

2. Nitawajalia amani katika familia zao
3. Nitawafaraji katika magumu yao yote
4. Nitakuwa kimbilio lao salama wakati wa maisha yao, na zaidi sana katika saa yao ya kufa
5. Nitawapa baraka tele katika shughuli zao zote
6. Wakosefu watapata katika Moyo wangu chanzo na bahari ya huruma isiyo na mwisho
7. Waumini walio vuguvugu watakuwa na bidii
8. Waumini wenye bidii watakwea kwa upesi katika ngazi za juu za ukamilifu
9. Nitabariki kila mahali ambapo picha au sanamu ya Moyo wangu Mtakatifu itawekwa na kuheshimiwa
10. Nitawajalia mapadre karama ya kuigusa mioyo migumu
11. Wale wote watakaoeneza Ibada hii kwa wengine majina yao yataandikwa ndani ya Moyo wangu na sitawasahau kamwe